

# MIAKA 50 YA UHURU WA TANZANIA

# NA




# MAPINDUZI YA KILIMO CHA KAHAWA

TANZANIA COFFEE BOARD

# Miaka 50 Ya Uhuru wa Tanzania

# Na

## MAPINDUZI YA KILIMO CHA KAHAWA



## 1961 - 2011

Bodi ya Kahawa Tanzania
S. L. P 732
Moshi, Tanzania

www.coffeeboard.or.tz
info@coffeeboard.or.tz

© Bodi ya Kahawa Tanzania 2011



**Tumethubutu, Tumeweza, Tunasonga mbele**

# YALIYOMO

*Bodi ya Kahawa Tanzania - TCB*.................................................. *vii*

*Dira, Azma na Misingi ya TCB*.................................................. *viii*

*Taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa Tanzania*......... *1*

*Kahawa Yetu*.................................................................................. *5*

*Historia ya Kahawa Nchini Tanzania (1700 – 1960)*.................. *8*

*Ukoloni na Kahawa ya Tanzania*................................................ *9*

*Kahawa na Miaka 25 ya Kwanza ya Uhuru*............................... *13*

*Uchumi wa dola kwenda Uchumi wa Soko*.................................. *21*

*Kahawa Katika Uchumi wa soko*................................................ *25*

*Uzalishaji Kuongezeka Zaidi ya Mara Dufu*............................... *34*

*Mabadiliko Katika Sekta Ndogo ya Kahawa (1961 - 2011)*.......... *39*

*Kahawa na Gharama za Uzalishaji*........................................... *43*

*Maeneo ya Kilimo cha Kahawa Tanzania*.................................... *46*

# Bodi Ya Kahawa Tanzania - TCB

Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB) ni Taasisi ya Umma iliyoundwa kwa sheria ya bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya bodi za mazao namba 23 ya mwaka 2001, ikiwa na majukumu yafuatayo:

- Kusimamia sekta ya kahawa Tanzania
- Kuishauri serikali mambo ya msingi juu ya mikakati ya kuendeleza kilimo na biashara ya kahawa
- Kutangaza sifa nzuri za kahawa ya nchi yetu kwa ajili ya kupata soko zuri na bei nzuri.

## Dira Yetu

TCB kuwa mfano wa usimamizi wa huduma bora katika sekta ya kahawa nchini Tanzania na bara zima la Afrika.

## Azma Yetu

Kuwezesha mazingira muafaka kwa maendeleo endelevu ya sekta ya kahawa nchini Tanzania.

## Misingi Yetu

Weledi, Ugunduzi, Tija na Uwajibikaji wa pamoja.



# USULI

## Taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa Tanzania

Historia ya kahawa Tanzania inaandikwa upya kipindi hiki cha maadhimisho ya miaka 50 ya uhuru wa Tanzania, mahsusi kwa lengo la kubaini mchango wa zao hili kwa uchumi wa taifa na kwa maendeleo ya jamii. Kadhalika, inatolewa kama sehemu ya taarifa ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika katika tathmini ya serikali juu ya mafanikio na changamoto za sekta ya kilimo katika harakati zake za kuwezesha maendeleo ya nchi.

Maadhimisho haya, yanayofikia kilele chake Dec 9, 2011 yanalenga kujenga mazingira muhimu kwa mwelekeo muafaka wa taifa letu kwa siku zijazo katika kupata namna bora ya kuondokana na changamoto mbalimbali zilizodumaza maendeleo ya nchi. Kwa mtazamo huo, yaliyomo katika kitabu hiki yanajaribu kuchambua changamoto na mafanikio ya sekta ndogo ya kahawa katika utekelezaji wa sera mbalimbali za kilimo kitaifa kuanzia zao la kahawa lilipoingia nchini kwa mara ya kwanza karne ya 18, na jitihada za serikali kwa kipindi chote tangu tulipokuwa taifa huru Dec 9, 1961 hadi tarehe 9, Dec 2011.

Katika kipindi cha miaka ya 1970 /80 Sekta ndogo ya kahawa ilikuwa mhimili wa maendeleo ya uchumi wa Tanzania kwa kuwapatia kipato cha moja kwa moja zaidi ya wakulima laki tano na kuajiri takriban watu wengine milioni 3.5 wanaolihudumia

zao hili katika nyanja mbali mbali kuanzia utafiti, ukusanyaji mashambani, usafirishaji, ukoboaji viwandani, ununuzi, uhifadhi maghalani na uuzaji wake sokoni hadi bandarini, tayari kusafirishwa kwenda nchi za nje.

Ingawa kwa zaidi ya miongo miwili (1990 na 2010) kilimo na biashara ya kahawa havikukua sawasawa na na matarajio ya nchi, kahawa imeendelea kuwa chanzo muhimu cha mapato ya fedha za kigeni yasiyopungua dola za kimarekani milioni 100 (Shs billion 170) kila mwaka, licha ya kuwa chanzo endelevu cha mapato ya fedha za kodi kwa serikali.

## Changamoto za Kilimo na Biashara ya Kahawa Katika Mifumo Miwili ya Uchumi Duniani

- 1961 – 1994 Ujamaa na kujitegemea, na
- 1994 – 2011 Uchumi wa soko /utandawazi.

Itakumbukwa kwamba kilimo cha kahawa kilianza nchini kibiashara katika mashamba makubwa ya Wakulima wahamiaji wa kizungu (walowezi) sanjari na utawala wa wakoloni. Kwa kuwa kahawa ni zao linalohitaji kazi nyingi za mikono ya binadamu, wananchi weusi katika makoloni, ndio walikuwa chanzo muhimu cha nguvu kazi iliyohitajika katika mashamba hayo, kiasi kwamba wafanyakazi walichukuliwa kutoka hata mikoa ya mbali kama Ruvuma, Iringa na Mbeya na waliwekwa kambini kama mali ya wenye mashamba hayo ambapo mmiliki aliweza kuishi mbali, akifika mara chache kukagua maendeleo ya shamba lake. Kilimo kwa mfumo huu kilijulikana (kwa lugha ya Kiingereza) kama ***serfdom*** *– yaani wafanyakazi wa mashambani kutumiwa kama sehemu ya mali ya wenye mashamba.*

**Kilimo cha wakulima wadogo:** Mfumo huo wa serfdom ulifanya wakulima wazawa kuwa na nafasi adimu kuweza kufanya kazi ya maana katika mashamba yao, uwezo mdogo kifedha wa kuwekeza katika kilimo cha kahawa, na mara nyingi kupigwa marufuku kuwa na mashamba yao wenyewe. Mambo yote hayo yalijenga misingi imara ya kilimo cha kahawa Tanzania kuwa cha vijishamba vidogo vya kujikimu tu.

### Fursa maalum

Uwepo wa maeneo makubwa (hadi) hekta milioni 4.8 zinazofaa kwa kilimo cha kahawa, (hekta laki 2 pekee zikiwa ndizo pekee zinazolimwa kahawa), kuendelea kukua kwa umaarufu wa aina zote mbili za kahawa ya Tanzania (Arabika na Robusta)

na, soko lililo tayari kuchukua kiasi kikubwa cha kahawa ya Tanzania (zaidi ya wastani wa tani elfu 50 zinazozalishwa kila mwaka kwa wakati huu) vinaifanya Tanzania kuwa na mazingira mazuri ya kuongeza uzaliushaji wa kahawa yake na kuuza kirahisi kwa faida kubwa.

Bila shaka tutayatumia vizuri maadhimisho haya ya kwanza ya miaka hamsini ya uhuru wa taifa letu kama nafasi pekee ya kujipanga upya, ili taifa liweze kuzitumia fursa hizo vizuri zaidi katika azma ya kuleta maendeleo endelevu, yasiyotegemezwa kwenye misaada ya mataifa mengine, kwani hiyo ndiyo tafsiri halisi ya uhuru wa kweli.

### Changamoto


Katika vipindi hivi (Ujamaa na Kujitegemea 1961 na Uchumi wa Soko 1994) changamoto mbalimbali zilizoiathiri sekta ndogo ya kahawa zilizojitokeza ni pamoja na: *Mabadiliko ya sera za kilimo na siasa ya nchi, hali ya hewa, mwenendo wa bei katika soko la kahawa la kimataifa, ufahamu mdogo wa mbinu za kilimo bora cha kahawa kwa wakulima wengi wadogo, na uwezo wao mdogo wa kiuchumi kuwekeza ipasavyo katika kuendesha kilimo na biashara ya kahawa kwa faida.*

## Mwelekeo wa Sekta ya Kahawa 2010 -2020


Jambo la kutia moyo katika kipindi hiki ni mwamko mpya unaoendelea kujengeka katika sekta ya kahawa unatokana na mabadiliko ya hivi karibuni ya kisera (Coffee Sector Reforms 2009) yaliyoidhinishwa na Bunge Mwaka 2009 na ambayo yameiwezesha bodi ya kahawa kupata nafasi zaidi ya ushirikishi wa wadau katika kuendeleza zao lao. Mabadiliko hayo tayari yanaonekana kuchochea ari mpya na shauku, si, kwa wadau wa kahawa pekee, bali pia kwa serikali yenyewe ambayo imeamua kugharamia baadhi ya mahitaji ya kilimo (pembejeo) kwa njia ya ruzuku, ilihali wadau wenyewe, licha ya kushiriki katika kujenga mkakati maalumu wa kuendeleza zao la kahawa (Coffee industry strategic Plan 2010 – 2020) waimeanzisha mfuko maalumu kuhakikisha fursa zilizopo zinatumika vizuri na kwa ufanisi mkubwa. Mkakati wa sekta ya kahawa unalenga kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa tani 50,000 za sasa kwa mwaka, hadi tani 100,000 katika kipindi cha miaka kumi ijayo.

Lengo la msingi ni kukuza mchango wa kahawa katika kipato cha wananchi na uchumi wa taifa kwa ujumla. Hii ndiyo hali tunayosherehekea nayo maadhimisho ya miaka 50 ya uhuru wa Tanzania.

# MATARAJIO YA UKUAJI WA SEKTA YA KAHAWA 2011 - 2021










Tumethubutu, Tumeweza na Tunasonga mbele

*Eng. Adolph A. Kumburu*

*MKURUGENZI MKUU*

# Kahawa Yetu



## Umuhimu wa Zao la Kahawa

Kahawa ni zao mhimili wa uchumi wa mamilioni ya watu ulimwenguni kote, wakinufaika na kilimo na biashara yake. Zao hili hulimwa katika nchi 47 barani Africa, Asia na Amerika ya Kusini. Tanzania ni miongoni mwa nchi 19 duniani, zinazozalisha aina zote mbili za kahawa - Robusta na Arabika.

Mamillioni ya watu wengine wanaonufaika na biashara pamoja na unywaji wa kahawa wako katika bara la Ulaya, Amerika ya kaskazini, Asia na kwa kiasi, katika bara la Afrika.


Zao la kahawa ndio bidhaa kubwa zaidi katika biashara ya kimataifa ikitanguliwa pekee na mafuta ya petroli na mazao yake, na kwa mantiki hiyo kuwa na umuhimu wa pekee kwa uchumi wa dunia.

## Mchango wa Kahawa kwa Maendeleo ya Taifa

Nchini Tanzania kahawa ni miongoni mwa mazao maarufu ya biashara ya kimataifa kwa zaidi ya karne moja kuanzia wakati wa utawala wa wakoloni wa kijerumani ikitoa mchango mkubwa kiuchumi. Biashara ya kahawa hulilingizia taifa zaidi ya wastani wa shilingi bilioni 170 katika mapato ya fedha za kigeni, licha ya kuwa mojawapo ya vyanzo vikuu vya mapato ya serikali katika fedha za kodi.

Kutokana na mchango huu mkubwa zao hili (kwa muda mrefu) limeendelea kutajwa kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa taifa, ilihali likiwa chanzo muhimu cha ajira kwa watanzania wanasadikiwa kufikia millioni 4; wanaojihusisha na kilimo chake, utafiti, huduma za ugani, utayarishaji (processing) na usafirishaji hadi bandari za Tanga na Dar es Salaam na kadhalika.

- *Chimbuko la mtandao mpana wa matawi ya mabenki katika wilaya nyingi zinazoendesha kilimo cha kahawa nchini na kupanua fursa ya ajira kwa maelfu ya watanzania wengine wengi,*
- *Shehena kwa meli zinazorejea nchi za nje baada ya kuleta nchini bidhaa kutoka nje na hivyo kusababisha kupunguza gharama za usfirishaji wa bidhaa zinazoingizwa na kutoka nchini,*
- *Fursa kwa matumizi ya magunia na kamba hivyo kutoa nafasi ya soko la bidhaa za katani inayolimwa kwa wingi nchini Tanzania.*




***Mchango wa Mazao Mbalimbali Katika Pato la Taifa***

Zao la kahawa lina nafasi pana ya kuchangia zaidi ya katika mafanikio ya malengo ya maendeleo ya nchi (pengine kuliko sekta nyingine yoyote) kutokana na;

- *Kuwepo maeneo makubwa wazi ya ardhi muafaka kwa kilimo cha kahawa. mathalan Tanzania ina zaidi ya hekta millioni 4.8 zenye rutuba na zinazofaa kwa kilimo cha kahawa katika maeneo mbalimbali nchini, huku kiasi kidogo tu cha hekta laki mbili pekee zikiwa ndizo zinazotumiwa kwa kilimo cha zao hili.*
- *Viwango vidogo vya uzalishaji visivyozidi gramu 200 kwa mti wa kahawa (kutokana na mbinu dhaifu za kilimo cha kahawa) ambao una uwezo wa kuzalishwa hadi gms 1000 (kilo moja) kwa kuboresha mbinu hizo,*



Shamba la Mkulima Mdogo Karatu Arusha

- *Uzoefu wa nchi wa zaidi ya karne moja katika kilimo cha kahawa,*

- *Uwepo wa soko kubwa katika nchi mbalimbali duniani lenye mvuto mkubwa kwa kahawa ya Tanzania huku nchi ikichangia kati ya wastania wa asilimia ndogo ya 0.8 - 1 katika uzalishaji wa kahawa duniani,*

- *Kuwepo kwa wawekezaji wakubwa, wakiwemo watanzania wenye uwezo wa kuwekeza katika maeneo mapya pamoja na uwezekano wa kufufua mashamba yaliyokufa katika maeneo aslia ya uzalishaji wa kahawakama Kilimanjaro na Arusha, na*

- *Utayari wa serikali ambayo imekuwa ikifanya mabadiliko mengi ya kisera (yakiwemo ya hivi karibuni (crops Boards Sector Reforms ya mwaka 2009) kuwekeza zaidi katika kuwapa nguvu wakulima wadogo na kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji kutoka nchi za nje.*

# Historia ya Kahawa Nchini Tanzania (1700 – 1960)



*Mb'uni wa Kahawa ya Robusta*

## Robusta

Kilimo cha kahawa kilianza nchini Tanzania karne ya 17 (mkoani Kagera), ambako kahawa aina ya robusta ililetwa na mashujaa wa kivita wa Bunyoro kutoka misitu ya Kongo, wakirejea nchini baada ya kushinda vita katika nchi za Jamhuri ya Afrika ya kati na Kongo Brazaville. Aina hii ya kahawa ilisitawishwa kwa mara ya kwanza kama mti wa jadi wa wafalme wa kabila la wahaya "Omuti gwo Mukama" ukichemshwa na kutafunwa katika mchanganyiko wa majani maalum, kwa imani za kuwalinda maaskari na madhara ya mapigano ya kivita. Kadhalika, ilitumiwa kama kitafunwa cha fahari na ushirikiano miongoni mwa watu wa hadhi kubwa mpaka mwanzoni mwa karne ya 20, kipindi ambacho ndicho walowezi wa kijerumani walipobadili kilimo chake kuwa cha kibiashara.

Kwa sasa robusta huchangia wastani wa asilimia 30 ya kahawa yote inayolimwa Tanzania. Asilimia 70 ya kahawa inayozalishwa Tanzania ni Arabika.

## Arabika

Kahawa ya Arabika iliingizwa nchini na wamisionari wa kifaransa kutoka Parokia ya "Bourbon" katika visiwa vya Re- Union kupitia bandari ya Kilwa na kusitawishwa bila mafanikio Matombo mkoani Morogoro mwishoni mwa miaka ya 1800. Jaribio la pili (miaka ya 1890) lilifanikiwa parokia ya Kilema kwenye miinuko ya mlima Kilimanjaro. Kilimo chake kilisambaa baadaye mikoa mingine ya Tanzania ikavuka mipaka na kuoteshwa kwa mara ya kwanza parokia ya mtakatifu Agustine huk Nyeri nchini Kenya.

Hadi mwaka 2011 kilimo cha kahawa kilikuwa kimesambaa katika mikoa 11 ya Tanzania Bara, ikiwemo mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Kilimanjaro, Arusha , Manyara, na Iringa, Rukwa, Kigoma, Tanga na Morogoro.

## Kahawa Kipindi cha Ukoloni

Kuingia nchini kwa walowezi wa kizungu (mwanzoni mwa karne ya 20) ambao walifungua mashamba makubwa ya kahawa, kulibadili sura ya kilimo cha kahawa kuwa cha mtazamo wa kibiashara. Kwa kuwa zao la kahawa hutegemea sana kazi za mikono ya binadamu, walowezi walihangaika kupata wafanya kazi hadi mikoa ya mbali kama Mbeya, Iringa na Ruvuma.

Aina hii ya kahawa ililimwa kwa nguvu kubwa za wananchi weusi wa Tanganyika. Mwaka 1910 wananchi walianzisha Kilimo cha kahawa katika mashamba yao mado-



*Mb'uni wa Kahawa ya Arabika*



*Shamba Kubwa la Kahawa Mkoani Kilimanjaro*

go kando kando ya mashamba ya walowezi. Wafanyakazi kutoka mikoa mingine walianza kilimo cha kahawa waliporejea makwao hususan matengo wilayani Mbinga mkoa wa Ruvuma na Mbozi mkoani Mbeya. Mikoa hii miwili ndiyo inaongoza nchini kwa sasa kwa uzalishaji wa kahawa ya Arabika.

Mwaka 1918 wakulima wa kiingereza waliwanyanganya mashamba wenzao wa kijerumani na kuunda chombo kilichosimamia Kilimo cha Kahawa cha walowezi kilichojulikana kama **Kilimanjaro Planters Association (KPA)**.

Hadi mwaka 1961 mwaka ambao Tanzania ilipata uhuru wake, jumla ya mashamba makubwa ya kahawa 172 (yenye eneo la hekta 2,200 - sawa na asilimia 10 ya eneo lote lililolimwa kahawa nchini wakati huo) yalikuwa yamepandwa kahawa nchini. Kitaifa kilimo cha kahawa kilisimamiwa na chombo kilichojulikana kama **Tanganyika Association of Coffee Traders Agency (TACTA)**. Mtazamo wa chombo hiki ulikuwa wa kulinda maslahi ya walowezi kwa kuhakikisha upatikanaji wa wafanyakazi /vibarua wa kiafrika.

Ilifika wakati wakulima wadogo wakazuiwa waziwazi kulima kahawa ili kuhakikisha upatikanaji wa nguvu-kazi katika mashamba makubwa. Vibarua hao walilipwa ujira mdogo kwa kazi nzito zilizohitajika katika kilimo, uvunaji na utayarishaji wa kahawa kwenye mashamba hayo ya walowezi. Wakati hayo yakiendelea kahawa ilizidi kupata umaarufu katika soko la dunia. Wafanyabiashara wa wakati huo (wengi wao wa asili ya kiasia - bara-hindi) waliuza kahawa kwa bei kubwa huku wakiwalipa wakulima wadogo bei ndogo isiyokuwa na tija. Serikali ya kikoloni haikujali maslahi

ya wananchi na mpaka wakati huu hapakuwepo chombo cha kufuatilia maslahi yao pamoja na kuwapatia taarifa za mwenendo wa bei ya kahawa katika soko la dunia.

Kazi nzito isiyokuwa na masilahi (katika mashamba ya walowezi na kilimo cha mashamba madogo kisichokuwa cha tija, vilididimiza hamasa na ari ya wakulima na wafanyakazi katika mashamba makubwa, na bila shaka hiyo ikawa ndio chanzo cha kushuka kwa morali ya kazi, hali iliyoifanya serikali ya kikoloni kuchukua hatua za dharura kunusuru Kilimo cha kahawa nchini.



*Sir. Charles Dundas*
*- Mwanzilishi wa kilimo cha kahawa kwa wakulima wadogo Kilimanjaro*

Hatua ya kwanza ilikuja mwaka 1919 wakati mtawala wa serikali ya kikoloni ya Kiingereza (Sir Charles Dundas) alipoamuru uhamasishaji wa kilimo cha kahawa mkoani Kilimanjaro. Hatua hiyo ikionekana dhahiri kutokupata mafanikio, mwaka 1925 serikali ililazimika kutunga sheria ya kuwalinda Wakulima wadogo. Sababu nyingine ya hatua hizi kuchukuliwa ni kuiwezesha serekali kulinda vyanzo vya mapato yake ya kodi na hasa ikizingatiwa kwamba wakati huo, kahawa ilikuwa ndilo zao muhimu la biashara la ukanda wa kaskazini mwa nchi. Kudhihirisha kwamba hali ilikuwa bado si shwari, wachagga waliunda ushirika wa kutetea maslahi yao uliojulikana kama Kilimanjaro Native Planters Asociation. Ushirika huo ukawa chimbuko la Vyama vya Ushirika vya msingi.

Hatimaye mwaka 1932 Wachagga wakaunda Chama Kikuu cha Ushirika (cha wazawa) – **Kilimanjaro Native Cooperative Union - KNCU Ltd**, kilichoandikishwa rasmi kisheria tarehe 29 Desemba 1933 na kuwa chama kikuu cha kwanza cha ushirika barani Afrika. Kuanzishwa chama hiki kulileta mabadiliko kidogo ya kimasilahi na hivyo kuwafanya Wakulima wadogo wa kiafrika kuendelea na kilimo cha kahawa.

Mkoani Kagera, wakulima wa robusta, (wakisukumwa na hali kama hiyo) waliunda ushirika wao – **Kagera Cooperative Union (KCU)** mwaka 1956. Hali iliendelea kuwa ya kusuasua kwa Wakulima wadogo ambao hawakuwa na uwezo wa kutosha wa kupanua Kilimo cha kahawa, msizitizo mkubwa ukibakia kulinda na kuhakikisha upatikanaji wa nguvu kazi kwa mashamba ya walowezi.

Mwishoni mwa miaka ya 1950 vuguvu la harakati za kupigania uhuru zikiwa zinaendelea kwa kasi, KNCU ilifanyiwa marekebisho na kuwa **Tanganyika Native Coffee Board**,- bodi ya kwanza ya kahawa nchini Tanganyika.

Makusudio ya chombo hiki yalikuwa kuwajengea wakulima wazawa:

*(a) Mazingira huru ya kumiliki mashamba yao,*
*(b) Ushiriki mpana na wenye tija katika Kilimo cha kahawa, pamoja na*
*(c) Usimazi wa sekta ya kahawa.*

Majukumu mengine ya Bodi hii yalikuwa;

*(d) Kuwaelimisha wakulima wadogo mbinu bora za Kilimo, na*
*(e) Kuhamasisha uzalishaji na ubora wa kahawa.*

## Tathmini ya Kilimo cha Kahawa Chini ya Utawala wa Kikoloni

Itakumbukwa kwamba kilimo cha kahawa (kibiashara) nchini Tanganyika kilianza kwa mfumo wa sera za kibepari, ziliozingatia maslahi ya serikali za kikoloni na wafanyabiashara kutoka katika nchi zao.

(i) Utawala huo uliwamilikisha walowezi mashamba makubwa na kuwaacha wazawa wakitumikishwa kazi nzito kwa ajira za muda mfupi zisizokuwa na maslahi.

(ii) Kadhalika walowezi walijengewa uwezo wa kuendesha mashamba makubwa, huku serikali ikifumbia macho haja ya kuwawezesha wazawa (watanzania). Hiyo ni mojawapo ya sababu za msingi zinazoelezea udogo wa mashamba ya wakulima wa kahawa nchini, hususan katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha ambako ndiko Kilimo cha kahawa kilianzia.

(iii) Athari nyingine muhimu ilikuwa ni nchi kupata mojawapo ya nguzo za uchumi wa fedha (cash economy) mfumo ambao umerahisisha biashara ya bidhaa mbalimbalimbali bila haja ya kubeba mizigo mikubwa ya mazao kwa ajili ya kubadilishana.

# Bodi ya Kwanza ya Kahawa Tanganyika Huru

## *Ujamaa na Kujitegemea* 1961-1976

Baada ya kutangazwa taifa huru Desemba 9, 1961, ikiwa ni hatua ya msingi kwa watanganyika kuanza mchakato wa kuendesha shughuhuli zao kwa ajili ya maendeleo yao na ya taifa lao, bila kuamuliwa na mtu au taifa lingine Serikali ilifanya mabadiliko ya mara kwa mara ya sera na kitaasisi kwa lengo la kuharakisha na uimarisha maendeleo ya kilimo na biashara. Mabadiliko ya kwanza kabisa yalikuja mwaka 1961 wakati serikali ilipotunga sheria ya kwanza ya sekta ya kahawa (Coffee Industry Ordinance 1961) iliyoiunda upya Bodi ya Kahawa mahali pa ile ya 1957 kutekeleza majukumu yaliyolenga kuboresha zaidi kilimo na biashara ya kahawa.




***Mara Baada ya Uhuru Serikali Ilibuni Stempu Maalum Kuhamasisha Kilimo cha Kahawa kwa Wakulima Wadogo***

### Majukumu na Shughuli za Bodi ya kwanza ya Kahawa Tanganyika

I. Kusimamia na kudhibiti sekta ya kahawa,
II. Kutoa elimu ya Kilimo bora cha kahawa kwa wakulima,
III. Kuishauri serikali (kupitia waziri wa Kilimo) hatua za kulinda na kuboresha ufanisi wa sekta ya kahawa (Kilimo na biashara yake),
IV. Kuhamasisha Kilimo cha kahawa katika maeneo mengi zaidi nchini, kuongeza uzalishaji na ubora wake,
V. Kuwakilisha taifa katika mikutano na matukio ya kahawa ya kimataifa ili kukuza sifa ya kahawa yetui na upatikanaji wa masoko ya uhakika.

## Azimio la Arusha na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea 1967

### Maudhui ya Azimio la Arusha na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea

- *Kuhakikisha ustawi wa raia wote kwa kuzuia mtu mmoja au kikundi kimoja kumnyonya/kukinyonya mtu mwingine au kikundi kingine,*
- *Kuona kwamba wakulima na wafanyakazi wanamiliki njia kuu za Uchumi na kuwa wanapata mgawanyo wa haki kulingana na kazi zao ,*
- *Kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo kama njia pekee ya kuleta maendeleo ya kweli, (kujitegemea kwa kuzallisha chakula cha kutosha na kuuza mazao mengi ya biashara kadiri ilivyowezekana) ili kulipatia taifa na wananchi wake fedha zaidi,*
- *Kuwaelimisha, kuwashauri na kuwaongoza wananchi vijijini kuwawezeshakutambua umuhimu na namna bora ya ushiriki wao katika shughuli za kujiletea maendeleo.*

Chama tawala - TANU na serikali yake viliweka mkazo katika matumizi bora ya rasilimali za taifa kwa faida ya wananchi. Kila mara msizitizo ulikuwa …“Kilimo ni uti wa mgongo wa maendeleo ya nchi” Siasa ni Kilimo, Uhuru na kujitegemea - uhuru na kazi, - baadaye, – “uhuru ni kazi” - misemo iliyotawala katika majukwa ya siasa na kwenye kila hotuba ya viongozi wakuu wa nchi.

Serikali ilitangaza vita dhidi ya Umaskini, Ujinga na Maradhi - maadui watatu wakuu wa uhuru wa Tanzania. Msingi wa mafanikio ……..ni wananchi kufanya kazi kwa bidii na maarifa. Kilimo cha kahawa kilipewa mtazamo na msukumo mpya wa kimasilahi kwa taifa na jamii.

Kuanzia Octoba 1, 1962 Bodi iliuza kahawa (Arabika iliyosafishwa) katika minada ya Moshi, wakati robusta na Arabika isiyosafishwa ziliuzwa katika minada ya Mombasa. Vyama vikuu vya Ushirika vilipeleka kahawa kwenye minada vikiwa vimeikusanya kutoka kwa Wakulima kupitia wanachama wake vyama vya msingi. Vyama hivyo vya msingi kwa kuwa karibu sana na wananchi vilikusanya kahawa kulingana na vijiji kahawa ilikolimwa na hivyo kuweza kulipa bei tofauti tofauti kulingana na ubora wa kahawa kwa mpango wa sehemu ilikozalishwa.

**Bei ya kahawa kwa mkulima ilitegemea mambo mawili:**

(a) Mwenendo wa bei katika minada na;
(b) Ubora wa kahawa ambao pia ulizingatia utaratibu wa sehemu kahawa ilikotoka (origin).

Utekelezaji wa hatua hii ulileta ufanisi kwa kuchochea utamaduni wa ushindani miongoni mwa wakulima. Kadiri mkulima alivozingatia kanuni za utunzaji bora wa kahawa na maandalizi yake baada ya kuvuna ndivyo alivyolipwa bei nzuri. Arabika laini ilikobolewa (cured) Tanganyika Coffee Curing Company (TCCCo) mjini Moshi, ilihali robusta na arabika isiyosafishwa zilipelekwa katika kiwanda cha Bukop Ltd mjini Bukoba.

Viwanda hivi viwili ndivyo pekee vilikoboa kahawa yote ya nchi nzima. Mwaka 1963 Serikali ilijenga kiwanda cha kusindika kahawa mkoani Kagera -'Tanganyika Instant Coffee Company (TANICA)' Limited kilichoanza kazi mwaka 1966 kikiwa na uwezo wa kuzalisha tani 500 za kahawa ya unga (instant coffee). Hadi mwaka 2011 TANICA Ltd ndicho kiwanda pekee mashariki mwa Afrika cha kuzalisha kahawa ya unga.

Serekali iliweka msizitizo katika huduma ya ushauri wa kitaalamu, ikaanzisha na kuvipa vyuo vya Kilimo changamoto ya kubuni mbinu bora za kitaalamu kumwongezea mkulima maarifa na ujuzi.




*Mashine ya elektroniki inayotumiwa kuendeshea minada ya kila wiki*

Wataalamu wengi walipelekwa vijijini walikofanya kazi kwa ufanisi mkubwa. Azimio la Arusha (lililotangazwa mwaka 1967) liliainisha dira ya taifa kuelekea maendeleo ya uchumi unaotegemea kilimo na utakaoletwa na Watanzania kwa usitawi wao na usitawi wa taifa lao.

**Matokeo ya Utekelezaji wa Sera ya Kilimo 1961 – 1977 (Ujamaa na Kujitegemea)**

- *Wakulima wadogo walipata msisimko na ari mpya ya kujituma zaidi na waliongeza kasi ya kuotesha kahawa na kuyatunza mashamba yao. Matokeo yake yakawa ni:*

- *Uzalishaji wa kahawa kuongezeka kutoka magunia laki nne (400,000) /tani 27,000 mwaka 1961 hadi magunia laki sita (600,000) /tani 36,000 mwaka 1970, wastani wa karibu 35000 kitaifa kwa mwaka katika kipindi cha miaka 10 baada ya uhuru,*

- *Umiliki wa wadau, wakiwemo wananchi wazawa,*

- *Kuanza kuenea kwa kilimo cha kahawa na kuimarika kwake katika mikoa ya Ruvuma hasa katika wilayani Mbinga na Mbozi mkoani Mbeya.*

- *Sekta ndogo ya kahawa kupata mwelekeo wa kitaifa,mchango wa Wakulima wadogo uki kua na kufikia zaidi ya wastani wa Asilimia 75 ya mavuno yote kitaifa,*


- *Kilimo cha kahawa kuanza kushamiri katika mikoa iliyokuwa inasua-sua kama Morogoro na Iringa na kusambaa maeneo mengine kama Kigoma na Babati huko Arusha,*

- *Uzalishaji wa kahawa kuongezeka hadi wastani wa magunia 900,000 (laki tisa ya kilo 60 kila moja) mwaka 1972 toka magunia 215,000 (laki mbili na elfu kumi na tano) mwaka 1962,*

- *Kuongezeka kwa mchango wa sekta ya kahawa kwa pato la taifa na kuwa moja ya mazao matatu makuu yaliyoliingizia taifa fedha nyingi zaidi za kigeni,*

- *Chanzo kikubwa cha ajira kwa mamilioni ya watanzania ambao ni Wakulima na wafanyakazi katika mtandao mpana wa kulihudumia zao na bidhaa ya kahawa.*

| Mwaka | Tani |
|---|---|
| 1961 | 24,600 |
| 1962 | 12,900 |
| 1963 | 24,600 |
| 1964 | 28,200 |
| 1965 | 30,600 |
| 1966 | 45,000 |
| 1967 | 49,200 |
| 1968 | 37,200 |
| 1969 | 57,000 |
| 1970 | 36,000 |




*Uzalishaji Kahawa Miaka 10 ya Uhuru - 1961 – 1970*

## Kutaifishwa Mashamba Makubwa ya Kahawa - 1973

Kukataa kwa wamiliki wa mashamba makubwa kulipwa asilimia 40 ya mapato ya kahawa (ya fedha za kigeni) kwa fedha za kitanzania na wao kubaki na asilimia 60 ya mapato hayo katika fedha za kigeni kuliichochea serikali kuyataifisha mashamba hayo, mengi katika mkoa wa Kilimanjaro.

Kwa mujibu wa taarifa za Serikali (zilizotolewa mara kwa mara kwa njia ya hotuba na vyombo vya habari),

**Mpango huo ulilenga kuliwezesha taifa:**

(1) Kupata fedha za kigeni bila ya kuwaathiri vibaya walowezi, serikali ikisadiki kuwa walihitaji na wangezitumia fedha za kitanzania kugharamia mishahara ya wafanyakazi, vibarua, miundo mbinu na pembejeo, ambazo, ama ziliagizwa na serikali kutoka nje ya nchi au zilizalishwa nchini,

(2) Uamuzi wa serikali unaonekana pia kushinikizwa na hali ya kisiasa ya wakati huo kukomesha unyonyaji na dharau ambayo wageni walionesha kwa wananchi mara kwa mara kwa kuwabeza. Serikali ilionekana kudhamiria kuonesha nia na uwezo wa kuwamilikisha wananchi njia kuu za uchumi.

(3) Kupoporomoka kwa biashara ya katani katika soko la dunia (kulikotokana na kugunduliwa kwa bidhaa za manila-synthetic fibre) kunaweza pia kuwa mojwapo ya vichocheo vya serikali kuchukua hatua hiyo ya kutaifisha mashamba ya kahawa. Itakumbukwa kuwa Tanganyika ndiyo ilikuwa inaongoza kwa uzalishaji wa katani duniani likiwa pia zao kuu la biashara kwa nchi yetu. Hii ndiyo sababu ya msingi ya kutumika kwa picha ya katani katika fedha ya Tanganyika ya wakati ule.

## Mamlaka ya Kahawa Tanzania

### *Coffee Authority of Tanzania (CAT) 1976 - 1984*

Kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, kuanguka kwa umuhimu wa katani katika soko la dunia na nia thabiti ya serikali ya kuimarisha mafanikio ya kilimo yaliyopatikana katika miaka ya 1960), bila shaka ni mambo yaliyoishinikiza serikali kuanzisha vyombo vya kuwashirikisha zaidi wananchi katika kuendesha na kusimamia shughuli za uzalishaji mali.

Kwa mtazamo huo Serikali ilianzisha Mamlaka ya Kahawa - CAT (1977 – 1984), majukumu yake yakiwa;

I. Kushirikisha wakulima wadogo na wadau wote wa kahawa katika utekelezaji wa sera.
II. Kutoa elimu ya kilimo bora cha kahawa na taarifa za masoko kuboresha mchango wa wananchi katika kuendeleza zao la kahawa,
III. Kuhamasisha kilimo cha kahawa maeneo mapya ya nchi, na kukuza viwango vya uzalishaji wa kahawa sehemu zote. Serikali iliipa CAT madaraka makubwa, sababu za msingi zikiwa ni;

(a) Kuhakikisha usimamizi na ufuatiliaji wa utendaji kazi vinatekelezwa ipasavyo na hasa kuona kwamba maofisa ugani wanatekeleza wajibu wao wa kuwashauri wakulima ipasavyo na;

(b) Kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kama ilivyokusudiwa. CAT ilitekeleza kwa ufanisi mkubwa mpango wa ruzuku uliofadhiliwa na serikali kwa ushirikiano na Jumuiya ya Ulaya (European Economic Community -EEC) chini ya utekelezaji wa miradi miwili ya Coffee Improvement Programme (CIP 1977 – 1981) na Coffee Development Programme (CDP 1982 – 1984).

Licha ya kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa mabwana na bibi shamba wa kahawa kwa nchi nzima, mradai wa CIP ulifadhili usafiri wa pikipiki kurahisisha usafiri kwa mabwana /bibi shamba.

- *CAT ilitengeneza vipeperushi, mabango na vitabu vya kuelimisha Wakulima vikiwa na picha, michoro na vielelezo vingi vya utunzaji bora wa shamba la kahawa, jinsi ya kutayarisha kahawa yenye sifa za ubora unaofaa, pamoja na faida za kutekeleza kila hatua kwa umakini. Serikali iliwawezesha wakulima wadogo kuongeza uzalishaji (kwa njia ya ruzuku ya pembejeo).*

- *CAT ilihusika moja kwa moja na elimu ya wataalamu wa kilimo cha kahawa ambao waliwasaidia wakulima vijijini ipasavyo. Kilimo kiliendeshwa kitaalamu kuwa cha kisasa na cha kibiashara,*

- *Vyama vya msingi vya Ushirika vilikusanya kahawa ya wakulima kwa niaba ya Mamlaka, ambayo iliiuza kahawa hiyo kwenye minada.*

- *CAT ilifungua ofisi za kanda katika mikoa ya Mbeya na Kilimanjaro na matawi katika wilaya kadhaa zilizolimwa kahawa, lengo kuu likiwa ni kuboresha mawasiliano na wadau na kuimarisha usimamizi. Kukamilika kwa muda wa utekelezaji wa miradi hiyo (CIP na CDP) ambayo ilikuwa nguvu kubwa ya CAT, kuliashiria pia mwisho wa Mamlaka hiyo.*

### Matokeo ya utekelezaji chini ya CAT (1977 – 1984)

- *Uzalishaji wa kahawa uliimarika (hususan katika mikoa ya Mbeya na Ruvuma). Kahawa ilipanda kwa umuhimu hadi kuongoza kama zao kuu la biashara Tanzania. Ingawa uzalishaji katika mashamba makubwa ulianguka (kutokana na serikali kushindwa kuyaendesha), wastani wa uzalishaji kwa mwaka kitaifa uliendelea kuongezeka na kufikia tani 51,000 (1971 – 1980), hili likiwa ongezeko la zaidi ya tani 16,000 kwa mwaka (tani 7000 juu ya tani 9000 kati ya 1961 – 1970) – uzalishaji ulipoongezeka kutoka tani 27,000 mwaka 1961 hadi tani 36,000 mwaka 1970.*


- *Kuongezeka kwa uzalishaji wa kahawa mwaka 1981, kufikia zaidi ya magunia milioni moja (1,000,000) - tani 64,000 magunia laki nane (800,0000) – tani 48,000 yakiwa arabika.*

- *Kukua kwa mapato ya kahawa kuliliwezesha taifa kuanzisha mipango ya ujenzi wa viwanda vya kukoboa kahawa vya Mbozi (Mbeya) na Mbinga (Ruvuma) kuongeza uwezo wa kukoboa kahawa (aina ya Arabika). Matarajio yalikuwa kwamba kasi ya uzalishaji kahawa kitaifa ingeendelea kukua hadi, au kuzidi tani laki moja (100,000 kwa mwaka). Viwanda hivyo vitatatu (kwa pamoja) na kile cha TCCCO ltd cha Moshi kilichojengwa wakati wa ukoloni vina uwezo wa kukoboa tani 150,000 kwa mwaka (vikifanya kazi kwa masaa 12 kwa siku),*

- *Mapato ya wakulima wadogo kuongezeka, kulikojionesha katika kuimarika kwao kiuwezo kugharamia elimu ya watoto wao na baadhi ya wakulima na wafanyakazi (maofisa ugani) wakijenga nyumba za kisasa.*

Katika kipindi hiki (1970 na 1980), kilimo cha kahawa kiliendelea kupanuka kwa kasi katika kanda ya kusini (Mbinga na Mbozi) kutokana na msukumo wa miradi ya Coffee Improvement Programme (CIP) 1977 – 1981 na Coffee Development Programme (CDP) 1982 – 1984 iliyogharamiwa na iliyokuwa Jumuiya ya Ulaya European Economic Community (EEC).

| Mwaka | Tani |
|---|---|
| 1971 | 54,000 |
| 1972 | 54,000 |
| 1973 | 67,200 |
| 1974 | 29,400 |
| 1975 | 55,200 |
| 1976 | 57,000 |
| 1977 | 48,000 |
| 1978 | 50,400 |
| 1979 | 52,800 |
| 1980 | 43,200 |




*Uzalishaji Kahawa Kipindi cha Miaka Mingine 10 ya Uhuru - 1971 – 1980*

Sera ilihimiza kilimo kwa kutumia teknolojia za kisasa kuwezesha uzalishaji kuongezeka. Aidha, ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wakulima wadogo, sera iliagiza kilimo kupitia mashamba ya bega kwa bega chini ya usimamizi wa Serikali za vijiji. Sera pia ilisisitiza uzingatiaji wa siasa ya kujitegemea kwa vijiji ili kubaini fursa za kilimo na kuamua shughuli za kufanya kwa ajili ya kujiletea maendeleo.

Jukumu kubwa la Serikali likawa ni kutoa msaada pale ulipohitajika. Vijiji vilihimizwa kuanzisha na kumiliki mashamba (communal farms) kama vyanzo vya mapato kwa ajili ya maendeleo yake. Sera ilitoa msukumo katika kuzingatia kanuni na mbinu bora za kilimo cha kahawa.

# Sera ya Taifa ya Kilimo (1983)

Sera hii ilihimiza kilimo kwa kutumia teknolojia za kisasa kuwezesha uzalishaji kuongezeka. Aidha kurahisisha utoaji wa huduma kwa wakulima wadogo, sera iliagiza kilimo kupitia mashamba ya bega kwa bega (block farms) chini ya usimamizi wa Serikali za vijiji. Sera pia ilisisitiza uzingatiaji wa siasa ya kujitegemea kwa vijiji kubaini fursa za kilimo na kuamua shughuli za kufanya kwa ajili ya kujiletea maendeleo. Jukumu kubwa la Serikali likawa ni kutoa msaada pale ulipohitajika. Vijiji vilihimizwa kuanzisha na kumiliki mashamba (communal farms) kama vyanzo vya mapato kwa ajili ya maendeleo yake.

Kwa zao la kahawa, sera ilitoa msukumo katika kuzingatia kanuni na mbinu bora za kilimo cha kahawa kuongeza uzalishaji na ubora wa mavuno yake.

## Bodi ya Masoko ya Kahawa

***- Tanzania Coffee Marketing Board (TCMB) 1984-1993***

Uhai wa CAT na miradi miwili mhimili wake (CIP na CDP) ilifikia ukingoni mwaka 1984. Kwa kutokuwa na uwezo wa kuigharamia CAT iliyopanuka nchi nzima na kuwa na matawi karibu katika wilaya zote zilizolima kahawa, Serikali ikaamua kubadili mbinu, ingawa lengo likibaki lile lile la kuboresha mchango wa kahawa kwa maendeleo ya taifa.

Mwaka 1984 serikali ilirejesha vyama vikuu vya ushirika na vya msingi kujiendesha vyenyewe kwa utaratibu wa awali, kuenguliwa mikononi mwa CAT na kuunda Bodi ya Masoko ya Kahawa (Tanzania Coffee Marketing Board -TCMB).

Kwa kupitia maafisa kilimo mikoani, Serikali ilisimamia uzalishaji wa kahawa na vyama vya Ushirika vikaendesha vituo vya mashamba darasa. Wakulima walikusanya kahawa na kuipeleka kwenye vyama vya msingi na kulipwa malipo ya awali (advance payment) kwa kutegemea bei ya mwanzo (indicative price) iliyotangazwa. TCMB iliendelea kutafuta na kuimarisha masoko (coffee promotion).

Wakulima waliendelea kukopeshwa pembejeo kuwawezesha kuzingatia utekelezaji wa kanuni za kilimo bora cha kahawa, wakati huu wakulima wakilipwa bei sawa bila kuzingatia tofauti za ubora, wakati gani wameuza kahawa yao na mahali inakotoka.


- Kahawa iliendelea kuwa mali ya mkulima hadi ilipouzwa kwa wanunuzi binafsi kwenye minada.

## Matokeo /Athari

Ingawa wakulima walifanikisha ujenzi wa viwanda viwili vya kukoboa kahawa nyanda za juu kusini, Mbozi Mbeya na Mbinga Ruvuma (kwa utaratibu wa makato kwenye mauzo ya kahawa yao) yale mafanikio ya kuongezeka uzalishaji wa kahawa (miaka ya 60 na 70) yalianza kuporomoka.

Katika kipindi cha miaka 10 (1985 – 1994) uzalishaji wa kahawa haukuendelea kukua kama ilivyokuwa miongo miwili kabla, badala yake ukashuka kutoka wastani wa tani 50,000 (1971 – 1980) hadi tani 49,700 (1985 – 1994) – miaka 10 baada ya miradi ya CIP na CDP.

| Mwaka | Tani |
|---|---|
| 1981 | 64,800 |
| 1982 | 55,034 |
| 1983 | 52,913 |
| 1984 | 47,053 |
| 1985 | 48,986 |
| 1986 | 53,975 |
| 1987 | 41,497 |
| 1988 | 49,049 |
| 1989 | 57,751 |
| 1990 | 53,320 |
| 1991 | 44,843 |
| 1992 | 48,008 |
| 1993 | 59,574 |
| 1994 | 34,152 |




*Uzalishaji Kahawa Kipindi cha 1981 – 1994*

Kuanguka kwa uzalishaji katika kipindi hicho kunaweza kukawa kukubwa zaidi hasa mafanikio ya CAT kiuzalishaji yanapotazamwa katika miaka mitatu ya mwisho wake. (1981 – tani 68,000, 1983 tani 55,800 na 1983 tani 61800) – ambao ni wastani wa tani 62,000 katika kipindi hicho cha miaka mitatu.



*Mashine ya Kisasa ya Kumenya Kahawa*

Ingawa Vyama vikuu vipya vya ushirika vilizaliwa hasa katika mikoa ya Mbeya - *Mbeya Coffee Cooperative Union* (**MBECCU**) LTD na Ruvuma - *Mbinga Coffee Cooperative Union* (**MBICCU**) LTD;

(i) Malipo kwa mkulima yalichelewa, wakati huo huo asilimia ya bei ya FOB kwa mkulima ikishuka.
(ii) Vyama vya ushirika vikiendeshwa kwa gharama kubwa bila uzoefu katika biashara na pia vikikumbwa na uendeshaji mbovu vilisababisha hasara kubwa.

Uzalishaji uliendelea kushuka hasa baada yaTCMB kuacha shughuli za uzalishaji, udhibiti wa pembejeo na upangaji wa bei.

## Sera ya Kilimo na Mifugo (1997)

Sera mbadala wa sera za Kilimo (1983) na Mifugo (1984), kufuatia nchi kutekeleza mageuzi ya kiuchumi kutoka uchumi wa dola kwenda uchumi wa soko. Sera inakiri kudorora kwa uzalishaji wa kahawa ambao umesuasua kwenye pungufu ya wastani wa tani 50,000 kwa zaidi ya miaka 25.

Hali hii ikitokana na sekta nzima ya kilimo kukabiliwa na matatizo ya ukosefu wa teknolojia ya kisasa; matatizo ya kifedha; viwanda kutotumika kwa uwezo wake na ubovu wa barabara za mashambani.

Ili kubadili hali hiyo Serikali iliamua kurejesha baadhi ya mambo yaliyotekelezwa wakati wa TCMB na CAT kwa kuunda Bodi ya Kahawa (TCB) na kuipa majukumu yafuatayo:-



*Mashine Kubwa ya Kumenya Kahawa (Pulper)*

(a) Kuelekeza huduma za ugani bila nguvu kubwa kwa wakulima wa kahawa;
(b) Kuruhusu makampuni binafsi kununua kahawa katika ngazi mbalimbali kwa lengo la kuboresha bei ya zao hasa kwa mkulima;
(c) Kushawishi wawekezaji binafsi kumiliki na kusimamia viwanda vya kati vya kumenya/kukoboa kahawa (Central Pulperies) kwa lengo la kuongeza ubora wa zao;
(d) Kuipa Bodi ya Kahawa mamlaka ya kisheria kuiwezesha kusimamia sekta ya kahawa; na
(e) Wizara ya Kilimo kupigania uimarishaji na matengenezo ya barabara za mashambani, hususan ni zile za mikoa mipya ya uzalishaji kama Mbeya na Ruvuma.

Utekelezaji wa sera hii ulisababisha hatua zifuatazo kuchukuliwa:-

(a) Kuruhusiwa ubinafsishaji wa pembejeo kama central pulpery units/hullers (viwanda vya kati vya kukoboa kahawa);

(b) Kubadilisha majukumu ya kitaasisi (crop board reforms 2009) ili kuhusisha serikali za mitaa, sekta binafsi na wadau wengine kushiriki kikamilifu katika jitihada za kuimarisha na kuendeleza sekta ya kahawa.

Mabadiliko haya yalipata nguvu ya kisheria baada ya mwongozo wa Waziri wa Kilimo na Chakula wa mwaka 2006. Bodi ya Kahawa ilipewa majukumu ya kiusimamizi (supervisory/regulatory functions) na majukumu shirikishi (shared functions), TCB ikigharamiwa na serikali kwa asilimia 100. Majukumu shirikishi yanatekelezwa na wadau wote kwa kushirikiana.

## Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDS)

Serikali iliandaa Mkakati wa Kuendeleza Kilimo nchini (Agricultural Sector Development Strategy - ASDS) kama sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Kilimo na Mifugo ya mwaka 1997, Dira ya Maendeleo ya Taifa na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini. Madhumuni ya ASDS ni kuweka mazingira bora kukifanya kilimo kuwa chenye tija.

Mkakati umebainisha vikwazo ambavyo wakulima wanakumbana navyo miongoni vikiwa ni sera zisizofaa, uhaba wa huduma za ugani, ukosefu wa mitaji, bei ndogo za mazao, ughali wa pembejeo, ukame, na miundombinu dhaifu. Katika kukabiliana na vikwazo hivi, mkakati unahimiza uwepo na umoja miongoni mwa wakulima kwa utaratibu wa vikundi (groups), vyama vya ushirika (cooperatives) na vyama (associations). Kwa mujibu wa ASDS, majukumu ya vyama vya wakulima ni:

- *Kutoa huduma kama vile taarifa, pembejeo, mikopo, uuzaji na ununuzi wa mazao;*
- *Kukusanya na kusambaza taarifa za masoko kwa wanachama;*
- *Kutoa elimu kwa wanachama kuhusu masuala ya uzalishaji wa kisasa na mahitaji ya masoko.*
- *Kutoa mafunzo juu ya masuala ya kiufundi na kimfumo; na*
- *Kutoa ushawishi na utetezi kwa kwa haki ya wanachama.*

Utekelezaji wa majukumu ya msingi (Regulatory functions) ya Bodi ya Kahawa unazingatia ASDS hususan katika eneo la kuwajengea uwezo wakulima wadogo wa kahawa (farmers empowerment) katika maeneo makuu yafuatayo:-

- *Kuwaunganisha wakulima (organizational empowerment);*
- *Kujenga ufahamu wa masuala mbalimbali yahusuyo tasnia ya kahawa (knowledge empowerment) kupitia mikutano ya kamati za kanda na mkutano mkuu wa wadau kila mwaka;*
- *Wakulima wadogo kumiliki miundombinu ya uzalishaji kama viwanda vidogo vya kumenyea/kukoboa kahawa (CPUs na hullers).*

Ili kubadili hali hiyo Serikali iliamua kurejesha baadhi ya mambo yaliyotekelezwa wakati wa TCMB na CAT kwa  kuunda na kuibebesha Bodi mpya ya Kahawa (TCB) majukumu kama ifuatavyo:-

(a) Kuelekeza huduma za ugani kwa wakulima wa kahawa;

(b) Kuruhusu makampuni binafsi kununua kahawa katika ngazi mbalimbali kwalengo la kuboresha bei ya zao hasa kwa mkulima;

(c) Kuipa Bodi ya Kahawa mamlaka ya kisheria kuiwezesha kusimamia sekta ya kahawa; na

(d) Wizara ya Kilimo kupigania uimarishaji na matengenezo ya barabara zamashambani, hususan ni zile za mikoa mipya ya uzalishaji kama Mbeya na Ruvuma.

## Bodi ya Kahawa Tanzania

***Tanzania Coffee Board (TCB) 1994 - 2001***

Ubinafsishaji na Uhuru wa Biashara Mwaka 1993, Serikali iliridhia utandawazi na kuruhusu uhuru wa soko na ubinafsishaji wa nyanja kuu za uchumi na kulazimika kubadili mfumo wa biashara ya kahawa na kutoa uhuru mkubwa kwa wafanyabiashara binafsi kununua mazao kutoka kwa wakulima. Mabadiliko hayo yalipunguza nafasi na uwezo wa Bodi ya Kahawa kudhibiti soko. Ushirika nao ukapata ushindani mkubwa kutoka kwa wafanyabishara binafsi. Mazingira haya yaliifanya serikali kubadili muundo mzima wa Bodi ya Kahawa. Kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 30, wanunuzi binafsi waliruhusiwa kununua na kukoboa kahawa katika viwanda vyao.

### Ubinafsishaji na Uchumi wa Soko *(Utandawazi 1994 - 2001)*

TCB kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya imeendelea kutoa leseni mbalimbali za biashara ya kahawa zikiwemo za:

(i) Kununua kahawa vijijini, ambako wafanya biashara binafsi wananunua kahawa kwa njia ya ushindani na vyama vya ushirika,

(ii) Lesseni za kukoboa kahawa (curing) kukaanga na kuuza nchi za nje na kadhalika,

(iii) Kuishauri serikali katika mambo yote yanayogusa maendeleo ya kilimo na biashara ya kahawa,

(iv) Kutangaza sifa ya kahawa nchi za nje na kujaribu kuhamasisha unywaji wake ndani ya nchi,

(v) Kuliwakilisha taifa katika mikutano na matukio muhimu (ndani na nje ya nchi) kwa mafanikio ya kilimo. Kwa kushirikiana na nchi za Kenya, Uganda na Ethiopia, TCB Ilihamasisha na kuandaa safari za wafanya biashara wakubwa (coffee roasters) maarufu kama East African Coffee Safari's), wakitoka Ulaya na Japan, na kwa kiasi fulani Amerika, kutembelea maeneo ya vivutio kwa watalii kama Ngoro ngoro, Serengeti, kupanda mlima Kilimanjaro na kutembelea mashamba ya wakulima wadogo. Kwa msaada wa Jumuiya ya Nchi za Ulaya EU, TCB:-

(vi) Iliandaa mabango, vipeperushi na kanda maalumu za video (kwa kiingereza, Kijerumani na Kijapani) vyote vikiitangaza sifa nzuri ya kahawa ya Tanzania nchi za nje;

(vii) Ilibuni na kutengeneza picha maalumu ya video ya mafunzo ya kilimo bora kwa wakulima wa kahawa – 'Ndoto ya Daudi" (drama) ambayo ilitumiwa na wataalamu wa kilimo kuwafundisha wakulima wa kahawa mbinu bora na faida zake kwa njia ya mvuto zaidi na pia kushawishi vijana wenye elimu kuwahamasisha kuingia kwenye kilimo cha kahawa.

- *Wakulima binafsi walianza kuruhusiwa kuuza kahawa moja kwa moja nchi za nje*
- *Bodi iliendesha minada ya kahawa kuhakiki bei na kiasi cha kahawa kilichouzwa nje ya nchi na biashara ya kahawa ya Tanzania.*

(viii) *Bodi iliendelea kupata mafanikio makubwa katika kutangaza sifa nzuri ya kahawa ya ukanda huu kwa kushirikiana na nchi nyingine za Afrika ya Mashariki na katika kwa uanachama wake wa chama kinachozijumuisha nchi za Ethiopia, Kenya, Uganda, Malawi, Zambia, Zimbabwe, Rwanda, Burundi, DR Congo, Angola na Tanzania) Eastern Africa Fine Coffees Association (EAFCA).*

## Matokeo ya Utekelezaji wa Mabadiliko ya Kisera na Kitaasisi

*(Kutoka Usimamizi wa Umma Kwenda Uhuru wa Soko)*

- *Ushindani wa (kibiashara) soko na hivyo kuongeza asilimia ya pato la mkulima.*
- *Wakulima kulipwa mazao yao papo hapo.*
- *Bodi ya Kahawa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja nataasisi ya utafiti wa kahawa (TaCRI) pamoja na Halmashauri za Wilaya zinazolima kahawa Tanzania, tumeweza kuandaa na kutekeleza mikakati ya ufufuaji na uendelezaji wa zao la kahawa ambapo uzalishaji wa kahawa umeongezeka kutoka tani 34,100 mwaka 2005/2006 hadi tani 68,000 mwaka 2008/2009.*
- *Kuongeza ubora wa kahawa katika daraja la kwanza hadi daraja la tano kutoka asilimia 32 mwaka 2002/2003 hadi asilimia 56% ya kahawa yote mwaka 2007/2008*
- *Kuhamasisha wakulima kujenga viwanda vya kati (central pulperies) ili kutoa kahawa yenye ubora wa juu na unaofanana. Hadi sasa viwanda vya kati (central pulperies) vipatavyo 250 vimejengwa nchi nzima.*

- *Kuandaa na kuendesha minada kwa njia ya electroniki ili kutoa ushindani mzuri wa soko kwa kuzingatia ubora na bei ya soko la kimataifa,*

- *Kutoa nafasi kwa Wakulima wa kahawa yenye ubora wa juu kuuza kahawa yao moja kwa moja nje ya nchi (direct coffee sale) ambayo hupata bei nzuri zaidi ya ile ya minada. Kahawa nyingi inauzwa katika masoko maalum (specialty coffee market) na wakulima wanaouza kahawa yao moja kwa moja nchi za nje wamefaidika na utaratibu huo,*

- *Kuongezeka kwa unywaji wa ndani kutoka asilimia 2% ya kahawa inayozalishwa nchini mwaka 2003 hadi kufikia asilimia 7% mwaka 2008*

- *Bodi ya Kahawa kwa kushirikiana na wadau wengine imehamasisha unywaji wa ndani wa kahawa kwa uanzishwaji wa mitambo binafsi ya ukaangaji, migahawa ya kahawa (coffee bars) nchi nzima ambazo zinaendeshwa na sektabinafsi,*

- *Bodi ya Kahawa imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa kutumia muundo wa utumishi wa mwaka 1999. Kutokana na mahitaji ya taasisi kuongezeka, bodi imeweza kubadili muundo wa utumishi ambao utaiwezesha kutekeleza majukumu yake kikamilifu.*


- *Bodi imekuwa ikiajiri watumishi kwa mujibu wa muundo huo mpya na kwa kadri ya mahitaji ya watumishi katika kada zilizoainishwa kila yatakavyojitokeza.*

- *Kwa upande wa mafunzo/kujenga uwezo, taasisi imekuwa ikitenga fedha ambazo hutumika kupeleka watumishi katika mafunzo ya muda mfupi.*

- *Dhana ya soko huru ghafla ikageuzwa na wengi na kutamkwa kama "soko huria" soko holela, (lisilokuwa na mipaka wala nidhamu). Wakulima wakajikuta kwenye mikono ya wafanyabiashara walaghai. Wafanyabiashara wazoefu walilazimika kuanzisha chama chao cha kahawa Tanzania (TCA) ambacho kimekuwa na umuhimu katika kulinda hadhi ya soko la kahawa ya Tanzania,*

- *Uzalishaji wa kahawa uliendelea kudorora kutoka wastani wa tani 49,700 kati ya mwaka 1985 na 1994 hadi tani 43,680 kati ya mwaka 1995 na 2004.*

| Mwaka | Tani |
|---|---|
| 1995 | 42,471 |
| 1996 | 52,304 |
| 1997 | 43,615 |
| 1998 | 37,812 |
| 1999 | 46,670 |
| 2000 | 47,811 |
| 2001 | 58,175 |
| 2002 | 37,923 |
| 2003 | 49,402 |
| 2004 | 33,789 |




*Uzalishaji Kahawa Kipindi cha 1995 – 2004*

Ongezeko la ghafla la viwanda vya kukoboa kahawa (10) vya makampuni/watu binafsi na kufanya uwezo wa kukoboa kahawa aina ya arabica inayosafishwa kufikia zaidi ya tani 200,000 licha ya uzalishaji kuendelea kupungua.

Kwa Robusta na Arabika isiyosafishwa viwanda viliongezeka kutoka viwili (vya umma) hadi viwanda 11 ambavyo vimeongeza uwezo wa kukoboa kahawa kwa zaidi ya tani 50,000 na kufika zaidi ya tani 110,000, huku uzalishaji wa aina hii ya kahawa ukiwa kwenye wastani wa tani 20,000 kwa mwaka.

## Tanzania Coffee Board (TCB) 2001 - 2009

Kwa mambo yalivyokuwa katika sekta hii, ilionekana wazi kuwa soko huru /huria lilivuruga dhana ya ushindani wa kweli katika soko la mnada, kwa kuwa wanunuzi shambani walikuwa na uhusiano na wanunuzi wa mnadani. Mwaka 2001 sheria ya kahawa ilibadilishwa na kuondoa mlolongo wa leseni kwa wafanyabiashara wa kahawa na kumpa nafasi mkulima kuuza mnadani na kupata bei kulingana na madaraja ya kahawa.

### Marekebisho Mengine

Kufufua shughuli za utafiti - maalum kwa zao la kahawa, (Utafiti) - wenye kumilikiwa na kugharamiwa na wadau wa zao wenyewe. Taasisi ya Utafiti wa Kahawa (TaCRI) ikaanzishwa mwaka 2001 – kubuni mbinu za kuongeza viwango vya uzalishaji na kupambana na magonjwa ya muda mrefu ya kahawa kama Chule buni – CBD, kutu ya majani na mnyauko fusari. Majukumu makubwa ya TaCRI yakaainishwa kama ifuatavyo:

- *Kuzalisha aina mpya za kahawa zenye viwango vikubwa vya uzalishaji na zenye uwezo wa kuvumilia CBD na magonjwa mengine ya kahawa,*




**Miche kutoka TaCRI ikioteshwa kwenye mashamba mapya**

- *Serikali ilianzisha soko la moja kwa moja nje ya nchi (Direct Coffee Export)kwa kahawa yenye kukidhi viwango vya ubora wa juu, spesheli.*

- *Kazi nzuri iliyofanywa na TACRI kugundua aina mpya zenye uwezo wa kuzaa zaidi, kustahimili magonjwa kama CBD na ambazo zimetumika kwa kiasi k ikubwa kubadili mibuni mizee ambayo imepitiliza muda wa kuzaa kiuchumi kumechangia kwa kiasi fulani kuanza kuongezeka tena kwa uzalishaji wa ka hawa na kufikia wastani wa tani 48,858 (wastani wa miaka 6) kutoka wastani wa tani 43,700 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho 1999 – 2004.*

- *Bila shaka mambo mengine ya msingi yaliyochangia mafanikio hayo kidogo ni pamoja na wakulima kufaidika na bei nzuri kwa kuuza moja kwa moja kwenye minada, kuongezeka kwa ubora wa kahawa, kwa kiasi fulani kunakotokana na kuthibiti hali ya ununuzi holela vijijini na utangazaji wa sifa nzuri ya kahawa ya Tanzania katika soko la dunia.*

| Mwaka | Tani |
|---|---|
| 2005 | 57,786 |
| 2006 | 36,434 |
| 2007 | 55,017 |
| 2008 | 44,745 |
| 2009 | 68,934 |
| 2010 | 35,668 |
| 2011 | 56,790 |




**Uzalishaji Kahawa Kipindi cha 2005 - 2011**

## Tanzania Coffee Board (TCB) 2009 . . .

Kutokana na sekta ya kahawa kuendelea kuyumba, au kutokupata maendeleo endelevu na ya kuridhisha mwaka 2008 serikali iliteua uongozi mpya wa TCB na kuupa jukumu maalumu la kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa marekebisho ya sekta ya kahawa yaliyopitishwa na bunge (Crops Boards reforms Act ya 2009).

**Marekebisho haya yaliweka mkazo maalum katika:**

(i) Kipengele cha shughuli shirikishi kwenye uendelezaji wa mazao ya biashara,

(ii) Serikali za Mikoa na Wilaya (LGA) kutambuliwa kuwa Mdau Na1 katika mikakati ya uendelezaji wa mazao,


(iii) Majukumu ya Bodi katika kusimamia na kuendeleza zao kulingana na program ya kuendeleza kilimo ya ASDP na kuboresha ushirika CRMP yameimarishwa,

(iv) Kuimarisha ushiriki wa wadau waliopo kwenye mipango ya kuongeza uzalishaji wa kahawa (wakulima na TaCRI)

(v) Upatikanaji wa takwimu za wakulima wa kahawa na kiasi cha kahawa inayozalishwa maeneo mbali mbali nchini ziboreshwe,

(vi) Ubora wa kahawa ya wakulima wadogo uboreshwe,

***Takwimu za Uzalishaji wa Kahawa Tanzania 1961 - 2011***



(vii) Kulifanyia kazi swala la matumizi ya mbolea katika uzalishaji wa kahawa na lile la kukosekana kwa takwimu za matumizi ya mbolea, na,

(viii) Ili kuhakikisha kuwa Bodi ya kahawa inaendesha shughuli zake kwa ulinganifu na wajibu /majukumu yake, kutazama upya mahitaji na uwezo wa Bodi.

## Mkakati wa TCB Kuongeza Uzalishaji na Ubora wa Kahawa 2011 - 2021

### A: Tathmini ya sekta ya kahawa (2008 /2009) kubaini fursa na changamoto za sekta ya kahawa;

Mwishoni mwa 2008 na May 2009 uongozi mpya wa TCB ulifanya utafiti katika mikoa 12 ya Tanzania bara. Utafiti huo ulibaini uwepo wa fursa pana na changamoto nyingi, ambavyo vikifanyiwa kazi kwa umakini mapato ya kahawa ya Tanzania yanaweza kuongezwa kwa zaidi ya maradufu ya yalivyo kwa sasa bila haja ya kutumia gharama kubwa. Kadhalika, matokeo ya utafiti huo ndiyo yalikuwa vigezo muhimu katika kuandaa mkakati wa kuboresha uzalishaji, ubora na mapato ya kahawa kwa kipindi cha 2011 – 2021 (Coffee Industry Development Strategy 2011 – 2021).

### Vigezo hivyo ni:

(i) Viwango vidogo vya uzalishaji wa kahawa kwa mbuni (wakulima wadogo) vya wastani wa gramu 200 - 250 kwa Arabika, na gramu 400 - 500 kwa Robusta, vinavyoweza kuongezwa hadi gramu 1000 (kg 1)za kahawa safi kwa mbuni vikifanyiwa kazi ipasavyo, na hivyo kulifanya taifa kuongeza kirahisi uzalishaji wa kahawa zaidi ya mara dufu ya wastani wa tani 50,000 wa miaka 15 hadi sasa,

(ii) Uwepo wa maeneo makubwa nchini yanayofaa kwa kilimo cha kahawa na mengine yaliyolimwa kahawa ambayo aidha yametelekezwa au hayajatumiwa vizuri,

(iii) Bei ndogo kwa mkulima - chanzo cha kushuka kwa uwezo, motisha na morali ya Wakulima wengi kuwekeza katika kilimo cha kahawa nchini,

(iv) Uwepo wa soko kubwa na lililo tayari kununua kahawa ya Tanzania kwa wingi na kwa bei nzuri zaidi, ilimradi nchi izalishe kahawa nyingi na iliyo bora zaidi,

(v) Uhakika wa Wakulima kuweza kuongeza uzalishaji na ubora wa kahawa, ilimradi wajengewe uwezo zaidi wa kuwekeza katika kilimo cha kahawa na kadhalika kupewa nafasi zaidi ya kushiriki katika maamuzi muhimu yanayogusa maendeleo ya kahawa.

## B: Kuongeza uzalishaji

Baada ya kutathmini fursa na changamoto za sekta ndogo ya kahawa Bodi ya kahawa iliingia hatua ya pili ya kuuandaa mkakati wa utekelezaji (bango kitita) kuongeza uzalishaji na ubora wa kahawa ikizingatia vigezo muhimu kama vifuatavyo:

(i) Ushiriki wa wadau wote muhimu wa sekta ya kahawa katika kuuandaa mkakati wa sasa kuboresha kilimo na biashara ya kahawa (coffee industry implementation plan 2011 – 2021); Wadau wa kahawa walioshiriki katika mkutano mkuu wa kahawa – Novemba na Desemba 2009 (wa kwanza tangu mwaka 2006) ambao walijadili na kukubaliana utaratibu muafaka wa kuamsha ari na kuongeza tija katika sekta hiyo ni – Wawakilishi wa Wakulima wa kahawa - vyama vikuu vya ushirika, asasi na jumuiya za wakulima waKahawa, chama cha wafanyabiashara wa kahawa Tanzania – TCA, Serikali za mitaa, taasisi ya Utafiti wa kahawa Tanzania - TaCRI na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.



*Aina Mpya ya Kahawa ikiwa Shambani*




*Shamba la majaribio TaCRI*

(ii) Wadau hao kwa pamoja walijadili na kukubaliana njia mbalimbali pamoja na kuweka nguvu zao kwa pamoja ili waeweze kutumia fursa zilizopo kuongeza uzalishaji na bora wa kahawa kama ifuatavyo;

*(a) Kupanua eneo la kilimo cha kahawa kutoka hekta 200,000 za sasa hadi 300,000 katika mikoa 6 mipya ya Manyara, Mwanza, Tanga, Morogoro, Iringa na Rukwa,*

*(b) Kuongeza uzalishaji kwa mbuni (wakulima wadogo) toka wastani wa gramu 250 za sasa hadi gramu 1000*

*(c) Kupanda mibuni mipya iliyofanyiwa utafiti na TACRI inayozaa zaidi na kuvumilia magonjwa ya chulebuni na kutu ya majani,*

*(d) Kuhamasisha kilimo cha mashamba makubwa kwenye maeneo yenye ardhi ya kutosha,*

(vi) Kugawa maeneo ya uzalishaji katika kanda za, Kaskazini Kilimanjaro na Arusha, Kusini: Ruvuma, Mbeya na Iringa, na Kanda ya Ziwa;- Kagera, Mara na Kigoma,

(vii) Kufungua ofisi za Bodi ya Kahawa katika kanda na kuwaajiri maafisa Kilimo ili wasaidie ushauri kwa wakulima na usimamizi wa karibu.

(viii) Kurejesha utaratibu wa mikutano ya wadau ya kila mwaka.

## Usimamizi

- Kuhakikisha mawakala wanaopunja bei ya mkulima wanadhibitiwa kwa kutangaza bei elekezi katika maeneo ya uzalishaji ili kudhibiti utoaji wa leseni,
- Kushirikisha zaidi mamlaka yenye dola katika halmashauri katika kusimamia kanuni za Kahawa na kuteua wakaguzi wa kahawa kila Halmashauri inayolima kahawa.
- Kusajili wakulima wa kahawa nchi nzima na kuhimiza Halamashauri kutumia sehemu ya mapato yake ya kahawa kuendeleza zao,
- Kuhamasisha ujenzi wa vituo vya kumenyea kahawa za Arabica nchini kote ili kukuza ubora wa kahawa yetu,
- Kufanya utafiti wa ardhi katika maeneo ya uzalishaji ili kubaini mahitaji sahihi ya mbolea.
- Kuitangaza kahawa ya Tanzania (promotion) kitaifa na kimataifa kadiri ya ubora wake kulingana na maeneo ya uzalishaji (appellations). Mfano kahawa za kusini zimeanza kuuzwa kwa jina la “Mbinga and Mbeya CPU” ikimaanisha kahawa zilizoboreshwa kupitia viwanda vya kumenyea. “Kilimanjaro” kwa Kahawa za kaskazini, “Kigoma AA” kwa kahawa za kigoma na “Victoria Naturals/ Hards” kwa kahawa za kanda ya Ziwa, Bukoba Robusta na Tarime Arabica.
- Kutumia mfumo thabiti wa kukusanya taarifa kwa kuweka kipengele cha utoaji taarifa kama sharti.

## KIINI CHA MATUMAINI YA KUONGEZEKA UZALISHAJI KWA ZAIDI YA MARADUFU KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 10 IJAYO

Misingi imara iliyotumika kuuandaa mkakati wa sekta ndogo ya kahawa 2008 na 2009.

**Misingi hiyo ni:** Tathmini ya sekta ndogo ya kahawa (2008 – 2009) iliyobainisha fursa nyingi wazi ambazo hazijatumiwa hata kwa nusu ya inavyotakiwa,

- Mjadala (ushiriki mpana) wa wadau kuhakiki umuhimu wa kahawa kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na haja ya kuhakikisha jambo hilo linafanyiwa kazi ipasavyo, na,
- Kuwepo kwa soko kubwa lenye uwezo na uchu wa kununua kahawa nyingi

zaidi ya Tanzania, ilimradi taifa lizalishe kiasi cha kutosha na kilicho katika ubora unaokubalika kimataifa.

## Mambo mengine ya msingi:

a) Utayari wa serikali kutoa ruzuku ili kuwawezesha wakulima wa kahawa kuwekeza kama inavyopasa katika uzalishaji wa kahawa,

b) Mafanikio ya Taasisi ya Utafiti wa Kahawa – TaCRI katika kuzalisha na kuendelea kusambaza kwa wingi nchini, aina mpya za kahawa zenye uwezo wa kuzaa kwa wingi na zenye kuvumilia magonjwa hatari kama chulebuni (CBD) na kutu ya majani,

c) Kuweko kwa maeneo makubwa wazi ya ardhi inayofaa kwa kilimo cha kahawa, kuongezeka kwa wawekezaji wakubwa katika kilimo cha kahawa, kufufuka kwa mwamko miongoni mwa wakulima wadogo kunakotokana na bei ya kahawa kuendelea kuimarika katika soko la dunia na kadhalika kukua kwa utamaduni wa unywaji kahawa nchini ambao umetoa mchango mkubwa katika kuimarika kwa uchumi wa kahawa wa mataifa yanayoendelea kufanikiwa katika uzalishaji wa kahawa kama Brazil na Ethiopia.

d) Ushirikiano mkubwa wa wadau (Wafanyabiashara binafsi, vyama vikuu vya Ushirika na taasisi nyingine zinazowawakilisha wakulima, TaCRI, halmashauri za wilaya, Wizara na Bodi ya Kahawa kama ulivyojionesha tangu wakati wa kuujadili na kuujenga mkakati wa sasa wa kuongeza uzalishaji wa kahawa, na;

e) Mipango madhubuti ya TCB ambayo imejengwa katika misingi ya kujifunza kutokana na hali, makosa na mafanikio ya taasisi zilizotangulia - tangu na kabla ya uhuru, kuajiri wataalamu wenye uwezo, utayari wa menejimenti kujenga uwazi, uwajibikaji na moyo wa kujituma miongoni mwa wafanyakazi wake na utataratibu wa kufungua ofisi za kanda katika maeneo mbalimbali ya nchi kwa lengo la kupeleka huduma karibu na wakulima.

# Mabadiliko ya Taasisi za Usimamizi wa Sekta Ndogo ya Kahawa

Tangu uhuru wa nchi yetu, sekta ya Kahawa imekuwa ikisimamiwa na Taasisi mbalimbali ambazo zimekuwa zikibadilika kufuatana na mabadiliko ya sera ya serikali. Taasisi hizo ni Bodi ya Kahawa Tanganyika (1961-1976), Mamlaka ya Kahawa Tanzania (1976-1984), Bodi ya Masoko ya Kahawa Tanzania (1984-1994) na Bodi ya Kahawa Tanzania (1994 hadi sasa). Taarifa hii inachambua jitihada zilizofanywa na taasisi hizi katika kusimamia na kuendeleza sekta ya Kahawa kwa kuzingatia sera na mikakati ya Serikali katika vipindi husika.

Tangu uhuru wa nchi yetu, jitihada za Serikali katika kuendeleza sekta ya kahawa nchini zimesimamiwa kupitia taasisi mbalimbali za serikali. Taasisi hizo ni Bodi ya Kahawa Tanganyika (Tanganyika Coffee Board), Mamlaka ya Kahawa Tanzania (Coffee Authority of Tanzania) Bodi ya Masoko ya Kahawa Tanzania(Tanzania Coffee Marketing Board) na Bodi ya Kahawa Tanzania (Tanzania Coffee Board). Viongozi (Watendaji wakuu na Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi) waliosimamia maendeleo ya sekta ya Kahawa katika Taasisi hizo wameorodheshwa hapa chini.

| Mwaka | Jina | Kilichotokea |
|---|---|---|
| 1957 - 1977 | Tanganyika Coffee Board | Harakati za uhuru |
| 1978 - 1983 | Coffee Authority of Tanzania | Kuvunjika kwa jumuia ya afrika mashariki |
| 1984 - 1993 | Tanzania Coffee Marketing Board | Vyama vya ushirika kukusanya mazao na Bodi kuwa muuzaji |
| 1994 - 2001 | Tanzania Coffee Board | Kuingia kwa soko huru |
| 2001 hadi sasa | Tanzania Coffee Board | Sekta kuwa na shughuli na kuimarisha usimamizi wa biashara |

*Jedwali 4: Mabadiliko ya kitaasisi*

## Viongozi wa Taasisi za Sekta ya Kahawa 1961 - 2011

### I Bodi ya Kahawa Tanganyika (Tanganyika Coffee Board)

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1961-1963 | Ndugu | J.M Hunter | -Mwenyekiti |
| | Ndugu | J.S Kasambala | -Naibu Mwenyekiti |
| 1962-1978 | Ndugu | Obedi A. Makule | -Mwenyekiti |
| | Ndugu | Lawrence L. Rutahakana | -Meneja Mkuu |

### II Mamlaka ya Kahawa Tanzania (Coffee Authority of Tanzania)

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1978-1983 | Ndugu | Sangito Kaaya | - Mwenyekiti Mtendaji |
| 1985-1990 | Ndugu | Werner Kapinga | - Mwenyekiti |
| | Ndugu | Lawrence Rutahakana | - Meneja Mkuu |
| | Ndugu | J. Masanja | - Meneja Mkuu |
| | Ndugu | Emmanuel Msuya | - Kaimu Meneja Mkuu |
| | Ndugu | Mtalo | - Kaimu Meneja Mkuu |
| | Ndugu | J. Mhela | - Meneja Mkuu |
| | Ndugu | Alphonce Rulegura | - Meneja Mkuu |

### III Bodi ya Masoko ya Kahawa (Tanzania Coffee Marketing Board)

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1987-2001 | Ndugu | Edward K. Sannda | -Meneja Mkuu |
| | Ndugu | Werner Kapinga | -Mwenyekiti |
| | Ndugu | S. Kagasheki | -Mwenyekiti |
| | Ndugu | Edward Lowassa | -Mwenyekiti |
| | Ndugu | Leslie D. Omari | -Mkurugenzi Mtendaji |

### IV Bodi ya Kahawa Tanzania (Tanzania Coffee Board)

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2001-2008 | Ndugu | Leslie D. Omari | -Mkurugenzi Mkuu |
| | Ndugu | George Kahama | -Mwenyekiti |
| | Ndugu | H. Mongi | -Mwenyekiti |
| | Ndugu | E. Mulokozi | -Mwenyekiti |
| 2008 -2011 | Ndugu | Adolph Kumburu | -Mkurugenzi Mkuu |
| | Ndugu | Pius Ngeze | -Mwenyekiti |

## Bodi ya Kahawa Tanzania (Tanzania Coffee Board)

Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Kahawa Tanzania Dec 2008 - Dec 2011:


| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bwana Pius B. Ngeze | *Mwenyekiti* |
| 2. | Bwana Adolph Kumburu | *Katibu* |
| 3. | Bwana Anyimike Kapyela | *Mjumbe* |
| 4. | Bwana Amir Hamza | *Mjumbe* |
| 5. | Bwana Geoffrey Kirenga | *Mjumbe* |
| 6. | Bwana Godwin Lemilia | *Mjumbe* |
| 7. | Bwana Vedastus Ngaiza | *Mjumbe* |
| 8. | Bwana Obadia Ndossi | *Mjumbe* |

Menejimenti ya kipindi hiki inaongozwa na Mkurugenzi Mkuu (Director General - DG), akisaidiwa na Wakuu wa Idara tatu - ambazo ni kurugenzi za; Fedha na Utawala (Director of Finance and Administration - DFA), kurugenzi ya Maendeleo ya Kahawa na Uendeshaji (Director of Coffee Development and Operations - DCDO) na kurugenzi ya Ubora na Uhamasishaji (Director of Coffee Quality and Promotion- DCQP).




***Kahawa House*** (Mjini Moshi)***- Makao Makuu ya Bodi ya Kahawa Tanzania***

## Muundo wa Utumishi wa TCB



## Matarajio Sekta Ndogo ya Kahawa Miaka 50 Ijayo

Katika kipindi cha miaka 50 ijayo, bodi itaweka mkazo katika kuwabadilisha wakulima wa kahawa ili wazidi kuwa wajasiriamali na washindani na hatimaye kuwa nguzo kuu ya tasnia ya kahawa nchini Tanzania.

***Mambo mengine muhimu yatakayozingatiwa ni pamoja na:***

(a) Kuzingatia kanuni bora za kilimo - zitakazosaidia Tanzania kuongeza uzalishaji na ubora unaokubalika katika masoko ya ndani na ya nje,

(b) Kuanzisha na kuendeleza kilimo cha kahawa katika maeneo mapya, kuongeza usindikaji wa kahawa hapa nchini ili kuongeza thamani ya kahawa sokoni, kushirikisha zaidi wadau wote katika kuimarisha tasnia ya kahawa iwe endelevu na,

(c) Kujenga na kusimamia utamaduni wa umakini, uwazi na uwajibikaji miongoni mwa wale wote watakaopewa nafasi za kusimamia katika sekta ndogo ya kahawa.

## Kilimo cha Kahawa Kinalipa

Ili kilimo cha kahawa kiweze kuwa kinacholipa, mkulima anapaswa kulima kwa kuzingatia kanuni zote za kilimo bora cha kahawa bila kuruka hata moja. Tafiti zinazofanana juu ya tathmini ya gharama za uzalishaji zimeshafanyika kwenye aina za zamani na aina mpya za kahawa. Tafiti hizi zimeonesha Kuwa aina za zamani zinazalishwa kwa gharama kubwa ikilinganishwa na kahawa inayotokana na miche bora ya TaCRI ambayo ina faida kubwa ikilinganishwa na kahawa ya zamani.


Kwa kuzingatia mchanganuo huu kama inavyooneshwa kwenye majedwali Gharama za uzalishaji na mapato katika kilimo cha kahawa, namba. 5 na 6 na namba 7 - Faida mpya ndizo zenye faida zinapolinganishwa na zile za zamani.

| Matokeo | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kazi/Mahitaji | Kanda ya Kaskazini | | Kanda ya Kusini | | Kanda ya nyanda za juu Kusini | |
| | Aina za Zamani | Aina Mpya | Aina za Zamani | Aina Mpya | Aina za Zamani | Aina Mpya |
| Mrututu/Viuatilifu | 1,465,500 | 184,500 | 1,465,500 | 184,500 | 1,465,500 | 184,500 |
| Vifaa vya kufanyia kazi | 324,000 | 324,000 | 324,000 | 324,000 | 324,000 | 324,000 |
| Mbolea za viwandani | 712,000 | 1,105,780 | 712,000 | 1,105,780 | 747,000 | 1,206,670 |
| Mbolea za asili | 580,000 | 580,000 | 846,600 | 846,600 | 846,600 | 846,600 |
| Palizi | 180,000 | 180,000 | 180,000 | 180,000 | 180,000 | 180,000 |
| Upogoaji | 171,000 | 171,000 | 171,000 | 171,000 | 396,000 | 399,000 |
| Uvunaji | 168,000 | 333,000 | 168,000 | 333,000 | 168,000 | 333,000 |
| Usindikaji | 62,100 | 85,200 | 62,100 | 85,200 | 62,100 | 85,200 |
| Jumla ya gharama za uzalishaji kwa hekta | 3,338,600 | 2,639,480 | 3,752,200 | 2,906,080 | 3,865,200 | 3,049,870 |

*Jedwali 5: Gharama za uzalishaji na mapato katika kilimo cha kahawa*


| Matokeo | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kazi/Mahitaji | Kanda ya Magharibi | | Kigoma | | Mara | |
| | Robusta | Arabika | Aina za Zamani | Aina Mpya | Aina za Zamani | Aina Mpya |
| Jumla ya gharama za uzalishaji kwa kilo moja (TZS) | 625 | 1,682 | 4,701 | 1,922 | 5,407 | 1,816 |
| Idadi ya miti kwa hekitari | 1,587 | 1,331 | 1,331 | 1,331 | 1,331 | 1,331 |
| Uzalishaji kwa mti (Kilo) | 2.3 | 1 | 0.5 | 1 | 0.5 | 1 |
| Uzalishaji kwa hekitari (Kilo) | 3,650 | 1,331 | 667 | 1,331 | 667 | 1,331 |
| Bei ya Kahawa | 1,700 | 2,900 | 3,000 | 3,000 | 3,000 | 3,000 |
| MAPATO (TZS) | *6,205,000* | *3,859,900* | *2,001,000* | *3,993,000* | *2,001,000* | *3,993,000* |
| FAIDA (TZS) | 3,923,440 | 1,620,660 | -1,134,900 | 1,434,500 | -1,600,300 | 1,575,700 |

*Jedwali 6: Gharama za uzalishaji na mapato katika kilimo cha kahawa*




***Jedwali 7: Faida ya aina za zamani ukilinganisha na aina mpya***

# Sehemu Zilimazo Kahawa Tanzania






**Tanzania Coffee Board**
Jengo la Kahawa House, Railway street, S.L.P 732 Moshi, Tanzania,
Simu: +255 27 2752324, Nukushi: +255 27 2752026, Barua Pepe: info@coffeeboard.or.tz,
www.coffeeboard.or.tz